

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Ndugu Naseeb Mmbaga anawatangazia wakazi wote na wananchi kwa ujumla kuchukua tahadhari dhidi ya uwepo wa ugonjwa wa Dengue ulioripotiwa nchini na Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia ,Wazee na Watoto Waziri Umy Mwalimu.

Akielezea kuhusu uwepo wa vimelea vya ugonjwa huo nchini Waziri Mwalimu alisema "ugonjwa huu huenezwa na mbu aina ya Aedes mwenye virusi vya homa ya Dengue na hupendelea kuzaliana kwenye maji yaliyotuama karibu na makazi ya watu"Alisisitiza.

Imeelezwa Mbu aina ya Aedes ni weusi na wenye madoa madoa meupe yenye kung'aa hivyo amewasihi wananchi kuvaa nguo ndefu na kutumia chandarua chenye viwatilifu kila mara hata nyakati za mchana.



Muonekano wa Mbu aenezae Homa ya Dengue.

Manispaa ya Temeke inafanya jitihada za hali ya juu ili kuwanusuru wananchi wake dhidi ya ugonjwa huu wa Dengue kwa kutoa Elimu kwa umma kwa kutanabaisha wakazi wake katika viunga vyote namna ya kujikinga na homa ya Dengue na kuwasihi wananchi wachukue tahadhari pindi wapatapo dalili zinazoashiria homa hiyo na kuwahi katika vituo vya Afya kwa uchunguzi zaidi.

Dalili hizo ni kuumwa kichwa ,Homa Kali, Kuumwa misuli, Kutapika pamoja na maumivu ya viungo.

"Tunza Mazingira epuka Dengu"